JARIDA LA

TAASISI YA SARATANI OCEAN ROAD

JANUARI - OKTOBA 2024

TOLEO LA 001

ORCI OCEAN ROAD CANCER INSTITUTE

# MASHINE YA PET/CT SCAN YAKAMILIKA KWA 100%

- Inatumia mionzi dawa inayozalishwa na 'Cyclotron'
- Watu wajitokeza kwa wingi kuhitaji huduma

Haliuzwi



orci_tanazania taasisiyasarataniocеanroad oceanroad www.orci.or.tz 0748 771 460

# JARIDA LA TAASISI YA SARATANI OCEAN ROAD

## YALIYOMO


**Bodi ya wadhamini** ....................................Ukurasa wa 01

**Menejimenti** ........................................Ukurasa wa 02

**Kutoka kwa Mkurugenzi** ........................................Ukurasa wa 03

**Waziri mkuu mstaafu Mizengo Pinda atembelea ORCI** ........................................Ukurasa wa 04

**Tanzania bingwa mapambano dhidi ya saratani** ........................................Ukurasa wa 05

**Mashine ya PET - CT SCAN yafanikiwa kwa 100%** ........................................Ukurasa wa 06

**Mammography kwa uchunguzi wa saratani ya matiti** ........................................Ukurasa wa 07

**Dkt. Rashid atoa ushauri juu ya kuishi bila saratani** ........................................Ukurasa wa 08

**ORCI yachunguza uvimbe wenye Kg 10.8** ........................................Ukurasa wa 09

**Prof. Kaaya: Ujenzi wa kituo cha Saratani Mbeya ni muhimu** ........................................Ukurasa wa 10

**Bw. Zawadi Phares: Serikali imeongeza bajeti ya dawa** ........................................Ukurasa wa 11

**Ununuzi wa mashine ya CT-SCAN wapunguza foleni za wagonjwa ORCI - Dkt. Iramu** ........................................Ukurasa wa 11

**ORCI yashiriki Sabasaba** ...............................Ukurasa wa 12

**ORCI yanyakua vikombe viwili siku ya Mei Mosi** ........................................Ukurasa wa 12

**Maswali yaulizwayo mara kwa mara na majibu** ........................................Ukurasa wa 13

**Kituo cha Habari** ........................................Ukurasa wa 13




Muonekano wa jengo la Taasisi ya Saratani Ocean Road (Block D).



Mashine mpya kabisa ya X-ray ipo ORCI.



Mashine ya Mammogram inachunguza saratani ya Matiti.



Mashine ya Spect huchunguza Saratani ya mifupa, Figo na shingo.


## LIMEANDALIWA NA :-

Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma, Taasisi ya Saratani Ocean Road, S.L.P 3592 Dar Es Salaam Tanzania

## TIMU YA UHARIRI

Dkt. Julius Mwaiselage
Islam Mposso
Dkt. Crispin Kahesa
Dkt. Mark Mseti

## PICHA:

Masoud Kassanga

## WAANDISHI WA HABARI:

Erick Mbonike
Irene Mwasomola
Zuberi Manyinja
Maryam Erasto
Superius Ernest

## WASANIFU KURASA:

Islam Mposso (0783243468)
Nathanael Gilbert


Jarida hili ni mali ya Taasisi ya Saratani Ocean Road, hivyo chochote kitakachotumika kutoka kwenye Jarida hili kwa matumizi yoyote yale binafsi au popote pale, ni lazima uwasiliane na wahusika wa Jarida hili kwa kupata Ruhusa ya matumizi hayo, ASANTE!

# BODI YA WADHAMINI



PROF. EPHATA KAAYA
MWENYEKITI



PROF. NAJAT MOHAMED
MJUMBE



PROF. BRUNO SUNGUYA
MJUMBE



DKT. OMARY UBUGUYU
MJUMBE



BI. AL-SHYMAA KWEGYIR
MJUMBE



BI. PRUDENCE MASAKO
MJUMBE



DKT. KIJAKAZI MASHOTO
MJUMBE



ADV. FRANCIS KAYICHILE
MJUMBE



PROF. MOHAMED JANABI
MJUMBE

# MENEJIMENTI



**DKT. JULIUS MWAISELAGE**
Mkurugenzi Mtendaji



**DKT. MARK MSETI**
Mkurugenzi Huduma za Tiba



**DKT. CRISPIN KAHESA**
Mkurugenzi Huduma za K-inga



**SR. MARY HAULE**
Mkurugenzi Huduma za Uuguzi



**DKT. ASAFU MUNEMA**
Mkurugenzi Huduma Saidizi za Tiba



**BI. BEATRICE ERASTO**
Mkurugenzi Utawala na Rasilimali watu



**CPA. GABRIEL SUNGI**
Mkurugenzi Fedha na Mipango



**ADV. ELIPENDO KAZIMOTO**
Mkuu Kitengo cha Sheria



**CPA. BENEDICTO NDALAHWA**
Mkuu Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani



**DKT. SADIQ SIU**
Mkuu Kitengo cha Ukaguzi Afya na Ubora wa Huduma



**BW. ISLAM MPOSSO**
Mkuu Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma



**BI. FLORENCE MKINGA**
Mkuu wa kitengo cha ununuzi na ugavi



**DKT.NAZIMA DHARSEE**
Mkuu wa kitengo cha tafiti na mafunzo



**BW. JOSHUA MMARI**
Mkuu wa Kitengo cha Tehama



**ENG. REGINALD MATOLA**
Mkuu wa Kitengo Ufundi na Usimamizi Miliki



# KUTOKA KWA MKURUGENZI

Karibu katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road iliyopo Ilala Dar es Salaam. Hii ndio taasisi maalumu inayotoa huduma za kiuchunguzi na matibabu ya saratani kulingana na majukumu yaliyoagizwa kwa kuzingatia sheria iliyoanzisha Taasisi.

Kupitia Sheria Na 3 ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilianzisha Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI) mwaka 1996, majukumu ya Taasísi hii kama ilivyoelekezwa katika sheria, ni pamoja na kusimamia masuala ya saratani hapa nchini, kuendesha hospitali ambayo inahudumia wagonjwa wa ndani na nje, kutoa matibabu kwa wagonjwa wa saratani, kutoa mafunzo ya Saratani, kufanya utafiti, na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu saratani.

Majukumu mengine ya TAASISI ni kutoa ushauri wa masuala yanayohusu saratani na kutekeleza majukumu mengine yanayohusu saratani

Dira ya Taasisi hii ni "kuwa cha ubora na sifa ya kitaifa, kikanda na kimataifa katika udhibiti wa maradhi ya saratani."

Dhamira ya Taasisi hii ni "Kutoa huduma bora za udhibiti wa saratani ambazo ni sawa, zinazofikiwa na kila mtu na nafuu kupitia kinga, uchunguzi na matibabu ya saratani, utafiti na mafunzo kwa kushirikiana na wadau."

Utoaji wa huduma za saratani katika kufikia dira na dhamira yetu unatekelezwa na wafanyakazi wenye weledi, ari na bidii katika kazi pamoja na utalaamu, unaoongezewa na miundombinu ya kisasa ya utoaji wa huduma za saratani.

Taasisi inajivunia kupanuka kwa kasi katika uwezo wa huduma, tayari Taasisi vifaa vya kisasa vya uchunguzi na matibabu ambavyo vinaboresha huduma zanazotolewa katika Taasisi, hivi karibuni Taasisi imekamilisha kusimika na kujaribu PET CT scan pamoja na Cyclotron ambazo ni mashine za kisasa kabisa katika uchunguzi wa saratani.

Upatikanaji wa dawa za tiba ya saratani ni 100% kwani dhamira ya Serikali ya Tanzania ni kuhakikisha wagonjwa wote wanaohitaji dawa wanapata bila usumbufu.

Dhumuni la Jarida hili ni kuelezea shughuli ambazo Taasisi imezifanya katika kipindi husika na pia kutoa elimu ya Saratani kwa wananchi ili waweze kuelewa kwa urahisi.

Kama wafanyakazi wa Taasisi hii, tumejitolea kulitumikia taifa katika kufikia ilani ya chama tawala na malengo ya maendeleo ya Tanzania 2025 ambapo lengo ni Upatikanaji wa huduma bora za afya ya msingi na matibabu ya kibingwa kwa wote.

# WAZIRI MKUU MSTAAFU MIZENGO PINDA ATEMBELEA ORCI, AKOSHWA NA HUDUMA ZAKE








Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Mizengo Pinda ameitembelea Taasisi ya Saratani Ocean Road mnamo tarehe 01/07/2024 jijini Dar es Salaam na kujionea uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali ya awamu ya sita katika uchunguzi na matibabu ya Saratani nchini.

Pamoja na maeneo mengine Mhe. Pinda amepata fursa ya kutembelea sehemu za Pet/CT Scan, Cyclotron, kwenye Mashine za CT, MRI kisha kupata elimu na uzoefu kutoka kwa wataalamu wanaotoa huduma katika maeneo hayo.

Aidha Mh. Pinda amewatembelea wagonjwa mbalimbali wakiwemo watanzania na wagonjwa waliotoka nchi za jirani ambao wamelazwa katika Taasisi hiyo. Pamoja na hayo Mhe. Pinda ametoa pongezi kwa watumishi wa Taasisi ya Saratani kwa kuendesha shughuli za kuwahudumia wagonjwa wa Saratani kwa weledi na kuwasihi uwe mwendelezo katika kuunga jitihada za Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan katika kuimarisha ustawi wa watanzania.

> "Hongereni sana Taasisi ya Saratani Ocean Road mnafanya kazi nzuri sana, mana furaha hii ya wagonjwa ni kielelezo kuwa kazi ni nzuri, endeleeni na kazi hii ili kuendeleza gurudumu la kuunga mkono jitihada za Rais wetu kusaidia watanzania

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road Dkt. Julius Mwaiselage wakati akisoma ripoti ya Taasisi, amesema hivi sasa idadi ya wagonjwa wanaofika kupima afya zao na kupata matibabu ya saratani nchini wameongezeka kutokana na elimu inayotolewa huku wengi wao wakija pindi wanapokuwa katika hatua za awali za ugonjwa.

Dkt. Mwaiselage amesema kuwa, Taasisi ina vifaa vyote vya kisasa vya uchunguzi na matibabu hivyo huduma zote za saratani zinapatika katika Taasisi hiyo, hali inayoipa uwezo Taasisi hiyo kupokea wagonjwa kutoka nchi za jirani ikiwemo Malawi, Zambia, Kenya na nchi nyinginezo.



# TANZANIA BINGWA MAPAMBANO DHIDI YA SARATANI

"Napenda kuushukuru Uongozi mzima wa shirika la Global Health Catalyst kwa kuitambua Tanzania kwenye mapambano dhidi ya saratani na kiukweli tuzo hii itakuwa chachu ya sisi kuongeza weledi na jitihada kubwa katika kuhakikisha tunapambana dhidi ya ugonjwa huu".

Dkt. Julius Mwaiselage

Tanzania yapewa Tuzo ya Global impact award 2024 kwa kazi kubwa zenye matokeo chanya zinazofanywa katika mapambano dhidi ya saratani ikiwemo chanjo ya HPV kwa wasichana, uchunguzi wa saratani ya matiti na mlango kizazi, usimikaji wa mashine za tiba mionzi, mashine za uchunguzi za CT scan, pamoja na PET CT Scan.

Tuzo hiyo imepokelewa na Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel akimuwakilisha aliyekuwa waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu katika Mkutano wa wadau wa sekta ya afya wanaojihusisha na mapambano dhidi ya ugonjwa wa Saratani uliofanyika tarehe 08/06/2024.



Naibu waziri wa Afya Mhe. Godwin Mollel akiwa ameshika tuzo iliyotolewa na Global Health Catalyst

Tuzo hiyo ilitolewa na Shirika la Global Health Catalyst lenye makazi yake Washington DC, USA.

Dkt. Mollel, amesema Serikali inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuimarisha huduma za Afya nchini kwa kuboresha miundombinu, vifaa tiba vya kisasa na Wataalamu wa kutosha ikiwa ni jitihada za kupambana na ugonjwa wa Saratani.



Dkt Mollel pia ameongeza kuwa, Ushirikiano uliopo baina ya Serikali ya Tanzania na Marekani unasaidia kuboresha sekta ya afya na kusaidia watanzania kupatiwa matibabu ya ugonjwa wa Saratani hapa hapa nchini na kupunguza Rufaa za kwenda nchi za nje na kupelekea kupunguza gharama za matibabu kwa watanzania na kuongeza kuwa ushirikiano huo unalenga kukuza Tiba Utalii ndani ya nchi ya Tanzania.



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road Dkt Julius Mwaiselage, amelishukuru shirika la Global Health Catalyst kwa kutambua mchango wa Tanzania kwenye mapambano dhidi ya Saratani na kusema kuwa Tuzo hiyo ni chachu ya kuongeza mapambano hayo.

Taasisi ya Saratani Ocean Road ni Taasisi pekee kubwa ya serikali ya Tanzania ambayo inatoa huduma za Saratani kwa wananchi wa ndani na nje ya nchi, ambapo kwa sasa imeendelea kuboreshwa kwa kuongezewa mashine mbalimbali za kisasa ili kupambana na ugonjwa huo.

# MASHINE YA PET CT SCAN YAFANIKIWA KWA 100%




*Picha mbalimbali zikionesha Mashine ya PET CT SCAN ilivyofanyiwa majaribio, mifumo ya TEHAMA ya uongozaji wa mashine hiyo Pamoja na wataalamu wakifanya majaribio hayo.*

Taasisi ya saratani Ocean Road kwa mara ya kwanza imefanikiwa kwa asilimia mia moja kufanya uchunguzi wa Saratani kwa kutumia mashine ya PET-CT SCAN.

Taarifa hiyo imetolewa na Dkt. Bright Sangiwa tarehe 24/05/2024 wakati akieleza mafanikio hayo ya Taasisi ya Saratani Ocean Road katika kuchunguza uwepo wa Saratani kwenye mwili wa binadamu ambao umechochewa baaada ya kufanikiwa kutengeneza dawa mionzi katika kiwanda cha dawa kilichopo ndani ya Taasisi kwa kutumia mashine ya CYCLOTRON.

Wakati akitoa maelezo ya mafanikio hayo Dkt. Bright amesema kuwa mashine ya PET-CT SCAN ina camera maalum ambayo inaweza kutumika kuchunguza uwepo wa saratani katika hatua za awali kabisa pale ambapo mgonjwa hajui ni wapi Ugonjwa ulipo huku dawa hiyo ya mionzi ikitumika kuchochea upatikanaji wa matokeo chanya.

"PET-CT SCAN ina camera inayotumika kuchunguza saratani katika hatua ya awali kabisa pale ambapo mgonjwa hafahamu ugonjwa ulipo, na mgonjwa anapopata kipimo hicho itasaidia kufanya uchunguzi zaidi ikiwa ni pamoja na kupata sampuli itakayoweza kujua ni Saratani ya aina gani" Ameeleza Dkt. Bright.

Vile vile ametoa wito kwa Wananchi wa Tanzania pamoja na wageni kutoka nje ya Nchi kufika katika Taasisi ya Saratani Ocean Road kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi kwenye mashine ya PET-CT SCAN.

Aidha Dkt. Bright ametoa shukrani zake za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusaidia upatikanaji wa mashine hizo katika Taasisi kwani imetoa heshima kubwa kwa taasisi, na hivyo kwa mara ya kwanza imeweza kuzalisha dawa Mionzi ambayo imeipelekwa kwenye matumizi katika mashine ya PET-CT SCAN ambayo imekubaliana na mionzi hiyo kwa asilimia Mia moja.

Mafanikio ya utengenezaji wa dawa hiyo ni hatua moja muhimu sana kuelekea matumizi thabiti ya mashine ya PET-CT SCAN kitendo ambacho kitapunguza safari za nje kufuata huduma hiyo kwa wagonjwa na hivyo kupunguza matumizi makubwa ya pesa za serikali.

# MAMMOGRAPHY NI MUHIMU SANA KWENYE UCHUNGUZI SARATANI YA MATITI - MKOLOMA

"unapofikisha umri wa miaka 40, unashauriwa na wataalam kufanya uchunguzi wa matiti kwa jinsia zote angalau mara moja kila mwaka. Hii itakusaidia kujua hali ya afya na kuKufanya uishi kwa amani". Bw. Mkoloma



*Mashine ya Mammography inayotumika kufanya uchunguzi wa saratani ya matiti*



"Sio wanawake tu hata wanaume wapo katika hatari ya kupata Saratani ya matiti hivyo uchunguzi huu unawahusu wote ili kuhakikisha usalama wao"

Mammography ni moja kati ya mashine ambazo zinapatikana katika Taasisi ya Saratani Ocean Road ambazo hutumika kufanya uchunguzi wa saratani ya Matiti ambapo msimamizi wake ni Bw. Steven Mkoloma

"Kumbukeni pia kipimo hiki hakina madhara yoyote hivyo ni vyema kufanya uchunguzi wa matiti mara kwa mara." Bw. Mkoloma

Bw. Mkoloma amezungumzia mashine hiyo na kusema kuwa kuwa huduma hiyo ya Mammography hutolewa kwa jinsia zote, wanawake na wanaume, kulingana na hali halisi ya ugonjwa jinsi ulivyo.

Bw. Mkoloma amefafanua kuwa huduma ya uchunguzi wa matiti kwa kutumia Mammography hutumia mionzi yenye kiwango kidogo kabisa, ambacho hakiwezi kuleta madhara kwa mgonjwa huku lengo likiwa ni kufanya uchunguzi na kutoa majibu ya uhakika na kwa haraka kwa mteja.

Amesema, "unapofikisha umri wa miaka 40, unashauriwa na wataalam kufanya uchunguzi wa matiti kwa jinsia zote angalau mara moja kila mwaka. Hii itakusaidia kujua hali ya afya na kuKufanya uishi kwa Amani. Kumbukeni pia kipimo hiki hakina madhara yoyote hivyo ni vyema kufanya uchunguzi wa matiti mara kwa mara."

Kipimo hicho ambacho huchunguza tishu za kwenye matiti kuona Kama kuna matatizo yoyote ikiwemo viuvimbe katika matiti, kinapatikana hapa katika Taasisi ya Saratani Ocean Road.

Mafunzo haya ni endelevu na hufanyika kila siku ya jumatano ya wiki ili kukumbushana kuhusu mambo mbalimbali ya kitabibu na yale ya kawaida

# DKT. RASHID ATOA SOMO JUU YA KUISHI BILA SARATANI

## ● Ni katika siku ya Saratani Duniani ● Shughuli yafana















*Matukio ya picha mbali mbali katika siku ya maadhimisho ya saratani duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Mbagala zakhiem.*

Serikali imetoa rai kwa jamii kuchukua hatua za mapema kupima ugonjwa wa saratani, kufanya mazoezi na kufuata mtindo bora wa maisha, kwani kuna ongezeko kubwa la wagonjwa, huku asilimia kubwa ya waathirika wakiwa ni wanawake.

Akizungumza katika maadhimisho ya siku ya saratani duniani tarehe 4/02/2024 Mkurugenzi wa Huduma za Afya na Ustawi wa Jamii kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Dk. Rashid Mfaume, amesema hadi kufikia mwaka 2030 athari za saratani zitakua mara mbili zaidi hasa katika nchi zenye kipato cha chini.

Pia amemshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa uwekezaji mkubwa alioufanya katika Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), ambapo ametoa zaidi ya shilingi bilioni 18 za ununuzi wa vifaa tiba.
Alisema kutokana na uwekezaji huo, kuna wagonjwa kutoka Zambia, Comoro , Msumbiji , Burundi na Kenya ambao wanafika ORCI kupata matibabu.

Naye Mkurugenzi mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dk. Julius Mwaisalage, amemshukuru Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa ununuzi wa mashine ya kisasa ya uchunguzi wa saratani (PET CT SCAN).

Dk. Mwaisalage amesema ORCI inaendelea kusimamia utoaji huduma za kibingwa kuanzia kinga na uchunguzi huku akisema, maadhimisho ya siku ya saratani mwaka huu yana kauli mbiu isemayo 'Saratani inatibika huduma sawa kwa wote.

Naye Mwakilishi kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) Dk. Alphoncia Nanai, amesema katika kipindi cha mwaka 2022 kwa ukanda wa Afrika wagonjwa wa saratani walikua ni zaidi ya 800,000, huku takribani 600,000 wakipoteza maisha.

Shughuli hii imeambatana na uzinduzi wa mchezo wa Afya game ambapo kwa shilingi 500 tu utachangia mgonjwa wa Saratani huku ukijiweka katika nafasi ya kushinda pikipiki, Nyumba na simu, mchezo huu umeandaliwa na wamata kwa udhamini wa Infinix.

# ORCI KWA MARA YA KWANZA YACHUNGUZA UVIMBE WENYE KG. 10.8

Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI) kwa mara ya kwanza imepokea sampuli ya uvimbe wa ovari wenye uzito wa kilogramu 10.8 kutoka hospitali ya rufaa ya mkoa wa Lindi ambao uligundulika kutoka kwa Mama mwenye umri wa Miaka 75, kwa ajili ya kuufanyia uchunguzi vile vile kujua ni nini kimesababisha kuwa mkubwa kupita kiasi.



Dkt. Angel Mlole akikata vipande kadhaa vya uvimbe huo ili kurahisisha uchunguzi wake.

Hayo yamebainishwa na Dkt. Asafu Munema, Mei 21, 2024 baada ya kupokea uvimbe huo kutoka Hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Lindi na kuanza kuufanyia uchunguzi alipokuwa kwenye Maabara ya Patholojia katika Taasisi ya Saratani Ocean Road.

Dkt. Munema ameeleza kuwa Maabara hiyo pamoja na uchunguzi wa uvimbe huo pia inafanya uchunguzi wa Viuvimbe vingine kutoka kwenye mwili wa binadamu ili kubaini kama vina Ugonjwa wa Saratani au laah!



Pichani ni uvimbe wenye zaidi ya kilo 10, uliotolewa kwa mgonjwa tayari kwaajili ya uchunguzi wa Saratani (Picha imezibwa kutokana na sababu za kimaadili).

Wakati wa uchunguzi wa sampuli hiyo, Dkt. Munema ameeleza kuwa sababu kubwa ya kuufanyia uchunguzi uvimbe huo ni kwa sababu umekuwa mkubwa kuzidi yai la uzazi la Mwanamke ambalo limeonekana kuwa si hali ya kawaida kwa binadamu.

Pia amesema kuwa hiyo ni hatua nzuri ya Ushirikiano mzuri uliopo baina ya Taasisi ya saratani na Hospitali nyingine ambazo zinahitaji uchunguzi wa saratani kwa wagonjwa wanaofika kwao.

"Hii imetokana na ushirikiano mzuri uliowekwa kati ya Taasisi ya Saratani Ocean Road pamoja na Hospitali za Rufaa za Mikoa ambapo mara nyingi Taasisi hiyo hufanya huduma za mkoba zilizoasisiwa na Rais wa Jamhuri ya Muunqano wa Tanzania Dkt. Samia, Ameeleza. Vile vile Dkt. Munema ametoa wito kwa wananchi wote kuwa wafike katika vituo vya Afya vilivyoko kote nchini ili waweze kujua hali za afya zao.

Taasisi ya Saratani Ocean Road imekuwa ikifanya uchunguzi wa sampuli ya vivimbe lakini safari hii imeweka rekodi kwa kufanya uchunguzi wa sampuli ya uvimbe wenye uzito mkubwa zaidi.

## HUDUMA ZA MAABARA

Huduma za maabara zimezidi kuimarika ambapo Katika kipindi cha miaka 3 cha awamu ya sita ambapo vipimo vya histopathology, cytology, Immunoassay (tumor markers), haematology, clinical chemistry, immunology, parasitology, na blood transfusion vinafanyika. Taasisi ilitoa, jumla ya vipimo 198,734 vya maabara ikiwa asilimia 96 ya lengo.

Vipimo mahsusi vya saratani tofauti tofauti vinafanyika hapahapa katika Taasisi ya Saratani Ocean Road na husaidia kutoa tiba mahsusi na ya kibingwa kwa wagonjwa wa saratani.

Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya 6, maabara ya Taasisi ilifanyiwa tathmini ya ithibati ya Kimataifa na kupewa ithibati katika vipimo vya aina tano kutoka Shirika la Viwango la Ukaguzi la Kimataifa (SADCAS).

hii inaonesha ni kwa kiasi gani huduma za kiuchunguzi zinaweza kushika hatamu katika maabara zetu kwani kwa kupata ithibati hii, imeweza kuongeza imani kwa nchi jirani kwenye suala la uchunguzi.

# PROF. KAAYA: UJENZI WA KITUO CHA SARATANI MBEYA NI MUHIMU


Prof. Ephata Kaaya


Ramani za ujenzi wa kituo cha saratani mkoani Mbeya kama inavyoonekana pichani

Taasisi itaanza utekelezaji wa jengo la kisasa lenye huduma za famasia, wodi za tiba kemia, wodi za binafsi, maabara na mradi wa ujenzi wa jengo la famasi na tiba kemia ambalo vyumba vya upasuaji. Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza huduma za upasuaji kwa magonjwa wa saratani katika Taasisi.

Mwenyekiti wa bodi ya wadhamini wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, Prof. Ephata Kaaya amesema kuwa kwa sasa, Taasisi imeanza utekelezaji wa mradi huu muhimu ambao utaweza kuhudumia wananchi wa mikoa 11 na nchi jirani zipatazo 6. Mikoa hiyo ni Mbeya, Iringa, Songwe, Njombe, Songea, Lindi, Mtwara, Kigoma, Tabora, Rukwa na Katavi. Nchi jirani za Malawi, Zambia, DRC, Msumbiji, Angola na Zimbabwe zitaweza kupatiwa huduma za kibingwa za uchunguzi na tiba ya saratani.

Prof. kaaya amesema utekelezaji wa kazi ulianza kwa kutangaza zabuni ya kumpata mkandarasi mshauri ambaye tayari amepatikana na amekamilisha michoro, zabuni ilikwishatangazwa na ushindani ulifanyika na Kwa sasa tayari mkandarasi wa ujenzi amekwishapatikana na utaratibu wa kuanza ujezi unaendelea,

Prof. Kaaya ametanabaisha kwamba Mradi huu utagharamiwa na Serikali ya awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Ujenzi huu ni muhimu sana kwani utaweza kusaidia wananchi wa kutokea maeneo jirani na mbeya badala ya kupoteza muda na Rasilimali fedha kutoka maeneo yao mpaka huku Dar es salaam, watatumia muda wao mchache kufika katika kituo hicho na kupata huduma sawa na zile ambazo wangezipata katika Taasisi ya Saratani Ocean Road amesema Prof. Kaaya na kumalizia kuwa huduma hii ni muhimu sana kwani, haitasaidia tu watanzania bali itafungua pia mipaka ya nchi za jirani na kuweza kuwasaidia




na hivyo kujenga uchumi imara na kuweza kujenga mitandao na watu wa nchi hizo na kuiingizia nchi yetu ya Tanzania pesa nyingi za kigeni.

# Bw. Zawadi Phares: SERIKALI IMEONGEZA BAJETI YA DAWA

Katika miaka ya nyuma, kero kubwa na malalamiko kutoka kwa wagonjwa ilikua ukosefu wa dawa za tiba kemia kwa ajili ya wagonjwa wa saratani.


Meneja wa kitengo cha Dawa katika Taasisi ya Saratani Ocean Road Bw. Zawadi Phares anasema katika Miaka ya hivi karibuni serikali ya Awamu ya Sita, imeweza kuongeza bajeti ya dawa za saratani kufikia TZS bilioni 10 kila mwaka kutoka TZS bilioni 6 za awali. jambo lililoimarisha upatikanaji wa dawa za saratani katika Taasisi kutoka asilimia 97 mwaka 2020/21 hadi wastani wa upatikanaji wa dawa asilimia 100 mwaka 2022/23 na kuendelea hivyo mpaka leo.

Bw. Phares anasema bei za dawa kwa wagonjwa wa saratani zipo chini kwa asilimia 30 katika maduka yetu yaliyopo ndani ya Taasisi, kulinganisha na maduka mengine ya binafsi.

Pamoja na hayo yote bado serikali kupitia Taasisi hii imeendelea kutoa dawa hizo kwa utaratibu wa misamaha ambapo wananchi wengi wamekuwa hawana uwezo wa kutosha hivyo hupatiwa dawa hizo kwa msaada.

Aidha Bw. Phares anatujuza kuwa, dawa ambazo zimekuwa zikitolewa kwa msaada ingawa zinagharimu pesa nyingi sana katika manunuzi yake ni pamoja na Tiba kemia, Tiba mionzi ambapo dawa hizi zimekuwa zikihitajika kwa kiasi kikubwa sana kwenye matibabu ya Saratani ili kuweza kurejesha hali ya mgonjwa katika uzima wa awali, hivyo kutokana na

''Bei za dawa kwa wagonjwa wa saratani zipo chini kwa asilimia 30 katika maduka yetu yaliyopo ndani ya Taasisi, kulinganisha na maduka mengine ya binafsi, hivyo ni nafuu zaidi.''


Bw. Zawadi Phares

utoaji huo wa misamaha mbalimbali kwenye dawa, jumla ya kiasi cha shilingi Bilioni 46,

hutumika kama misamaha kwa wananchi kila mwaka.

Taasisi inajitahidi kuhakikisha kila mtanzania anapata huduma za matibabu bila kujali kipato chake, anamaliza Bw. Phares.

## UNUNUZI WA MASHINE YA CT SCAN WAPUNGUZA FOLENI ZA WAGONJWA ORCI - Dkt. IRAMU


Dkt. Revelian Iramu

Dkt. Revelian Iramu ni meneja wa Radiolojia, katika Taasisi ya Saratani Ocean Road ametutanabaisha kuwa, Taasisi imenunua mashine mpya ya CT Scan yenye vipande 128 (slices) na kuweza kupanga matibabu ya mionzi ambapo usimikaji umekwishamalizika na ukarabati wa jengo lake na sasa imeanza kufanya kazi ambapo wananchi mbalimbali wameendelea kunufaika na huduma hii kutoka hapa Taasisi ya Saratani Ocean Road.

''Taasisi ilikuwa na mashine ya 3D moja tu ambapo mashine hiyo ilikuwa ikifanya kazi kwa kupokezana ikiwamo kufanya uchunguzi na kisha badae katika vipindi vya mchana itapanga matibabu ya mionzi, huku ile mashine ya 2D ikiendelea kufanya kazi kwa kusua sua kutokana na kuwa ni ya muda mrefu, hali hii ilipelekea kuwa na foleni kubwa sana kwenye utoaji wa huduma za CT Scan kwa wagonjwa''.Anasema Dkt. Iramu.

Baada ya serikali kuiona kadhia hiyo, ikaamua kununua mashine hii mpya na ya kisasa inayotumia teknolojia ya 3D ambapo Dkt. Iramu anasema, jumla ya shilingi bilioni 1.8 zimetolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa, Dkt Samia Suluhu Hassan.

Dkt. Iramu anatueleza kuwa kwa sasa foleni za kusubiria


Mashine mpya ya CT scan kwa ajili ya uchunguzi wa saratani

huduma hii ya CT Scan imekwisha, mteja akifika anahudumiwa anaondoka, hivyo watu wanakaribishwa kupata huduma hii kwa haraka na uhakika na kwa gharama nafuu ukilinganisha na Taasisi nyingine.

# ORCI YASHIRIKI MAONESHO YA SABASABA



Mkurugenzi mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road Dkt. Julius Mwaiselage (Mwenye Suti) akiongea na baadhi ya wateja waliotembelea banda la Taasisi hiyo, kwenye viwanja vya maonesho ya kimataifa ya kibiashara ya Saba Saba


Moja kati ya Wateja aliyetembelea banda letu, akifanya uchunguzi wa Saratani ya Tezi Dume

Taasisi ya Saratani Ocean Road kwa mara nyingine tena mwaka 2024, imeshiriki kwenye maonesho ya kimataifa ya Biashara ya Sabasaba ambayo yamefanyika katika viwanja vya maonesho hayo vilivyopo Temeke jijini Dar es salaam.

katika maadhimisho hayo Taasisi ya Saratani imefanikiwa kufanya uchunguzi kwa watu wasiopungua 400 ambapo uchunguzi huo umefanyika bila malipo, yakiwashirikisha madaktari bingwa kutoka katika Taasisi hiyo.

katika uchunguzi huo wale ambao walionekana kuwa na changamoto mbalimbali, walipewa rufaa na kuletwa katika Taasisi yetu na kupatiwa matibabu maramoja ili kuweza kunusuru Afya zao.

pamoja na huduma hiyo pia tulikuwa na huduma ya ushauri kuhusu Lishe bora, tiba shufaa na ushauri mwingine wa kitaalam kutoka kwa madaktari bingwa.


Wataalam wa huduma mbalimbali kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road (Wenye fulana nyekundu) wakimuelewesha jambo mteja aliyetembelea banda la ORCI kwenye viwanja vya maonesho ya kimataifa ya kibiashara ya Saba Saba

nafasi ya utoaji wa huduma kwa wananchi wanaohudhuria katika maonesho hayo imekuwa ni ya muendelezo na kuonekana kuwa imezaa matunda ya kupata wananchi wengi kwani, asilimia kubwa ya wananchi ambao hukosa muda wa kufika katika Taasisi yetu hupata muda hapa na kufanyiwa uchunguzi na kupewa majibu yao baada ya muda mfupi sana.

# ORCI WANYAKUA VIKOMBE VIWILI SIKUKUU YA MEI MOSI


Bw. Moshi Mteta (kulia) akipokea kikombe cha mshindi wa kwanza kwenye mchezo wa Bao kutoka kwa makamu wa Rais wa JMT Dkt. Philip Mpango katika maadhimisho ya Mei Mosi, mkoani Arusha

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya saratani Ocean Road Dkt. Julius Mwaiselage amepokea vikombe vya ushindi vya Taasisi ya Saratani Ocean Road katika mashimdano ya Mei Mosi Taifa 2024 yaliyofanyika tarehe 01/05/2024 mkoani Arusha.

Taasisi ya saratani Ocean Road imekuwa mshindi wa Kwanza katika mchezo wa bao kwa wanaume, huku ikishika nafasi ya tatu kwa wanaume kwenye mbio za baiskeli.

Dkt. Mwaiselage amewapongeza washiriki wote walio iwakilisha Taasisi katika mashindano hayo ya Mei Mosi huku akisema kuwa Taasisi ya Saratani ni kubwa na imebarikiwa kiasi kwamba pamoja na kutoa huduma za matibabu ya Saratani, wanashiriki na kushinda katika michezo mbalimbali. Dkt. Mwaiselage kipekee amewapongeza mshindi wa Kwanza wa Bao Bw. Moshi Mteta na mshindi wa tatu wa mbio za Baiskeli Bw. Stephen Sanga, huku akisisitiza wengine kuongeza juhudi ili wakati ujao tupate makombe mengi zaidi.



Ushiriki wa mazoezi kila jumamosi kama ishara ya kuunga mkono agizo la waziri mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa Ilimesisitizwa ili kujiweka katika sehemu ya kuimarisha afya za wafanyakazi.

ORCI OCEAN ROAD CANCER INSTITUTE



# MASAWALI YANAYO ULIZWA MARA KWA MARA NA MAJIBU YAKE

**Swali**
Serikali imeokoa kiasi gani kwa Taasisi hii kuboresha huduma zake kimatibabu?

**Jibu**
Serikali ilikuwa ikitumia shilingi bilioni nane kupeleka wagonjwa nie ya nchi, Iakini sasa kutokana na huduma kuendelea kuimarishwa fedha zinazotumika sasa ni Chini ya sh.milioni 200.

**Swali**
Mna míkakati gani ya kutoa huduma kwa wagonjwa wa mikoani kuepusha usumbufu hasa kwa wasio na uwezo kufika hapa?

**Jibu**
Wagonjwa tutakuwa tukiwa hudumia huko walipo míkoani, mgonjwa akipatikana tutakuwa tunashauriana na hospitali husika na kuwaelekeza vipimo vya kuwafanyia wagonjwa ili wanapofika katika Taasisi yetu wasitumie muda mrefu.

**Swali**
Mtu anapotaka kutíbiwa hapa ni bima gani ambazo zinakubalika?

**Jibu**
Aina za bima zinazopokelewa katika Taasisi hii ni NHIF, Jubilee Insuarance, Strategis, jeshi la Wananchi, JKT, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Puma energy. UNHCCR na Britam. Tuna mifuko zaidi ya IO ambayo tayari tumeingia nayo mikataba

**Swali**
Taasisi ipo "Buzy" kiasi gani kwa maana ya kutibia wagonjwa wale wanaotoka nie na huwa mnapokea wagonjwa wapya wangapi kwa siku?

**Jibu**
Tunatoa huduma za kuona wagonjwa wa nje 950 kwa siku. wagonjwa wapya ni 200 na wale wanaokwenda na kurudi ni 750. hii imefanva kuwa na watu wengi sana kwa siku ambao wanatutembelea. japokuwa pamoja na wingi huu, bado tunamudu kuwahudumia kila mmoja.

Je una maoni au maswali yoyote kuhusu Taasisi au ugonjwa wa Saratani? Tafadhali tuandikie kupitia, info@orci.or.tz au tupigie kupitia 0748771460

## INFORMATION CENTRE

Taasisi ya Saratani Ocean Road, imeweka sehemu maalum inayoitwa Information Center". Sehemu ambayo inawapa fursa wateja wanaofika katika Taasisi hii kuweza kuuliza na kujulishwa mambo mbalimbali yanayo husiana na maradhi ya Saratani pamoja na huduma zinazopatikana katika Taasisi

Kitengo hichi kinakuwa wazi siku ya jumatatu mpaka siku ya ijumaa kuania saa mbili kamili asubuhi mpaka saa kumi kamili jioni.




Bi. Jasmin Said (kulia) akiongea na mteja

Aidha Bi. Jasmin Said, ambae kwa sasa ndiye msimamizi wa kitengo hiki anasema kuwa kitengo hichi kimekuwa ni msaada mkubwa kwa wateja ambapo wamekuwa wakipata uelewa chanya kuhusiana na maradhi haya ya Saratani, kwa kuwaondoa hofu walizozipata kwa kusikia maneno ya mtaani kuusiana na maradhi ya saratani.

Wateja wamekuwa wakipata taarifa namna magonjwa ya saratani yanavyoenea mwilini na namna gani tiba zinafanyika katika Taasisi ya Saratani Ocean Road

Bi Jasmin alieleza kuwa katika kitengo chake uwa wanatoa matiti bandia kwa akina mama waiiokatwa matiti. Matiti hayo bandia hupewa kwa wale wenye uhitaji.




**TAASISI YA SARATANI OCEAN ROAD**

**S.L.P 3592, Dar Es Salaam,Tanzania**

**Barua Pepe: info@orci.or.tz**

**Huduma kwa mteja: +255 748 771 460** **Simu: +255-22-2127597**